## Masuala ya Msingi Katika Utayarishaji wa Majaribio kwa Wanafunzi Wanaojifunza Kiswahili kama Lugha ya Pili

*Y.I. Rubanza*

*Iksiri*

Karibu miaka 20 iliyopita, pamekuwa na utafiti na matumizi ya matokeo ya utafiti huo kuhusu majaribio yanayotolewa kwa wanafunzi wa lugha za magharibi. Hata hivyo, kwa upande wa Kiswahili utafiti huo wa majaribio haujafanyika ama kwa kina au haujafanyika kabisa. Lengo la makala haya ni kutafakari masuala ya msingi kuhusu suala la majaribio ya Kiswahili kwa wanafunzi wanaojifunza lugha hiyo kama lugha ya pili. Baadhi ya vipengele ambavyo vinazingatiwa katika makala haya ni pamoja na mtiririko na mchakato unaoathiri ufaulu wa majaribio hayo pamoja na uzingativu wa maadili ya upimaji huo. Hivyo basi, inapendekezwa kuwa majaribio yanayofaa ni yale yanayozingatia uthabiti unaoendana na maadili ya upimaji pamoja na malengo ya mawasiliano na ustadi wa lugha.

### 1.0 Utangulizi

Mchakato wa kutunga majaribio (dhana ya neno 'majaribio' katika makala haya itajumuisha testi, mitihani, mazoezi) ni mkubwa na tata. Hata hivyo, lengo kuu la majaribio hayo ni kupima maarifa au kiwango cha stadi wanazotarajia wanafunzi kuzijua katika lugha inayohusika. *Stadi hizo* zinazingatia masuala mbalimbali ya lugha pamoja na malengo ya wahusika, yaani walimu (watunga majaribio) na wanafunzi (wafanya majaribio). Hivyo basi, katika makala haya tutagusia sababu za utungaji wa majaribio, aina za majaribio na vigezo vya majaribio bora huku tukijiegemeza katika utungaji wa majaribio ya Kiswahili kwa wanafunzi wanaojifunza lugha hiyo kama lugha ya pili. Aidha, tunakiri kuwa katika makala haya tunazingatia ujuzi wa ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni katika chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Chuo hiki kimekuwa kikipokea wanafunzi mbalimbali kutoka nchi za nje, mfano, kutoka Afrika (Hususan Ghana na Libya), Marekani, Ujerumani, Italia, nchi za Skandinavia (Denmark, Norway, Sweden), Japani, China na Korea, kwa takriban zaidi ya miaka 20 hivi. Katika kipindi hicho chote, katika ufundishaji, walimu wamekuwa wakitunga majaribio ya aina mbalimbali. Makala haya yanadurusu juhudi hizo na mchakato mzima wa majaribio kwa ujumla na kupima mustakabali wake.

### 2.0 Aina za Majaribio

Kuna aina mbalimbali za majaribio yenye malengo tofauti. Kuna majaribio ya Kimataifa yanayopima viwango vya uelewa wa stadi kadhaa za lugha. Wanafunzi wanapofaulu hayo hutuzwa vyeti maalumu vinavyotambulika kimataifa. Baadhi ya lugha ambazo zina utaratibu wa kupima na kutoa vyeti vya

Kimataifa ni pamoja na Kichina, Kiingereza, Kifaransa, Kijerumani, Kijapani na Kikorea. Katika Kiingereza peke yake kuna mitihani ya aina nyingi kama vile: TOEFEL, TOEIC, IELTS, FCE, ESOL n.k. Mitihani ya TOEFL, kwa mfano, ilianzishwa miaka ya 1960 na inalenga kupima stadi za upokezi na utumizi wa lugha, uwezo wa kufahamu uyasomayo na uyasikiayo; inalenga kupima uwezo wa kuandika kwa kutumia lugha hiyo. Mitihani hiyo imetumika kupima uwezo wa wanafunzi wa Kimataifa ambao Kiingereza ni lugha yao ya pili au zaidi, hasa wanaotarajia kusoma katika vyuo vya Marekani. Kwa bahati mbaya hapajaanzishwa utaratibu wa aina hiyo katika Kiswahili, jambo ambalo tutalidokeza hapo baadaye.

Aina ya pili ya majaribio ni ile ya kupima maendeleo ya wanafunzi. Majaribio ya aina hii ndio yanayotumika kwa wingi katika madarasa ya Kiswahili. Mitihani hii hulenga kupima uzingativu wa kipengele maalumu cha silabasi (mwisho wa wiki, kwa njia ya mkupuo au mwisho wa muhula). Mitihani hii pia hupima maendeleo ya wanafunzi katika uwezo wa kukumbuka mafundisho ya darasani. Mara nyingi hulenga katika kumpa motisha mwanafunzi. Na kwa kawaida wanafunzi hupima maendeleo yao. Inawezekana kukawa na aina nyingine za upimaji lakini katika makala haya tutazingatia aina hizo mbili na kutafakari kwa kina aina hiyo ya pili. Majaribio tutakayoyajadili ni yale yanayotathmini Kiswahili kama lugha ya pili. Tathmini hiyo inaweza kufungamanisha stadi tano, yaani usikilizaji, uzungumzaji, usomaji, uandikaji na kupima uelewa wa utamaduni wa Waswahili. Kwa kawaida uzito wa upimaji huelekezwa katika utumiaji wa lugha, na kwa baadhi ya wanafunzi wenye malengo ya kuelewa lugha inavyofanya kazi kinadharia, upimaji huzingatia ufahamu wa lugha yenyewe. Hivyo basi, malengo ya majaribio hutofautiana kwa kuzingatia vipengele kadhaa ambavyo vitajadiliwa katika sehemu zinazofuata.

### 3.0 Majaribio bora

Majaribio ni taratibu za kupima uwezo, maarifa au utendaji wa wanafunzi. Kwa miaka mingi majaribio yametumika ili kumpatia mwanafunzi gredi (alama ioneshayo kiwango cha kufanikiwa au kutofanikiwa). Hata hivyo, mkabala huo unaonwa kuwa una dosari kwa kiwango fulani kwa kuwa, kama asemavyo Rivers (1968), utaratibu huo unaonesha *yale asiyoyajua mwanafunzi na yale ambayo hajafundishwa.* Jaribio zuri linapaswa kuonesha ujifunzaji wa mwanafunzi pamoja na matatizo aliyonayo katika ujifunzaji wake. Jaribio linamsaidia mwalimu kujua matokeo (mazuri) ya ufundishaji wake.

Wataalamu Bachman na Palmer (1996) wanaeleza kuwa, majaribio bora yanazingatia vipimo vya ubora vifuatavyo: uaminikaji, uthibitikaji, uhalisia,

uhusianifu, matokeo (yaliyokusudiwa) na utekelezekaji. Ufafanuzi wa sifa hizi kwa ufupi ni kama ifuatavyo:

(a) Jaribio linapaswa kuaminika au, kuleta matokeo yaleyale au yanayokaribiana nayo kila mara jaribio hilo linapofanyika katika mazingira tofauti. Ikiwa, kwa mfano, mwanafunzi anafanya jaribio mwanzoni mwa kozi na mwishoni mwa kozi, basi maendeleo yake yatokane na tofauti za stadi alizomudu na sio makosa aliyoyafanya katika jaribio hilo.

(b) Uthibitikaji unahusu mazingira ambamo wapimaji wanaweza kuelezea matokeo ya jaribio kama kiashirio cha uwezo wa wanafunzi wanaopimwa. Kwa hakika, jaribio linalothibitika ni lazima lipime kile kilichokusudiwa kupimwa.

(c) Uhalisia unahusu kufaa kwa matokeo ya watumizi wa lugha kama kifaa cha mawasiliano.

(d) Uhusianifu unaelezeka kama kiwango na aina ya uhusianishaji wa wanafunzi katika kufanikisha malengo ya jaribio linalohusika.

(e) Matokeo yanaelezeka kama njia mbalimbali za jinsi manufaa ya jaribio yanavyoathiri jumuiya au, kwa mfano, mfumo wa elimu na manufaa kwa mwanafunzi.

(f) Utekelezekaji unahusu uwiano wa rasilimali (yaani fedha na watu). Kwa mfano, mwalimu inabidi ajiulize jaribio atakalo wanafunzi wafanye litachukua muda gani? Matayarisho yapi yanahitajika? Je, vifaa gani vinahitajika n.k. Kwa hakika majaribio yanapaswa kuzingatia gharama za utayarishaji wake na uwezo wa kumudu gharama hizo.

Pamoja na vidokezo vya Bachman na Palmer (weshatajwa) kuna umuhimu pia wa kuzingatia uwezekano wa jaribio kuonesha matokeo ya aina moja licha ya kusahihishwa na watu mbalimbali. Kwa ufupi ni kwamba, mchakato wa usahihishaji usiathirike kutokana na haiba ya msahihishaji. Aidha, jaribio linapaswa kuwa limeandikwa kwa lugha nyepesi, ya wazi na sahihi. Mtunzi wa jaribio aepuke maswali na maelekezo yenye utata.

Kwa miaka ya hivi karibuni, yaani miaka ya 70 hadi mwanzoni mwa miaka ya 80 (Glenn Fulcher, 2000), majaribio mengi yamekuwa yakizingatia lengo kuu la ujifunzaji na ufundishaji lugha ambalo ni mawasiliano. Ufundishaji kwa mbinu ya kimawasiliano ni mbinu ya ufundishaji lugha ya pili au lugha ngeni inayosisitiza mawasiliano na maathiriano, kama njia tumizi na lengo kuu la ujifunzaji lugha. Kwa kuzingatia mbinu hii, lengo la ufundishaji lugha ni kumwezesha mjifunzaji kutumia lugha lengwa katika mawasiliano na katika mazingira halisi. Aidha, mbinu hii inamhitaji mfundishaji kutumia mazingira na matini halisi wakati wa ufundishaji huku akizingatia ujuzi wa wanafunzi kama

sifa ya lazima na muhimu katika mazingira ya ufundishaji. Hivyo basi, majaribio yanayozingatia mbinu hii lazima yajikite katika kupima utumiaji wa lugha katika mazingira halisi. Kwa hakika majaribio yanayozingatia mbinu ya kimawasiliano hayana budi kulenga utendaji (majaribio ya kiutendaji) na hivyo, hulazimu tathmini kufanywa wakati mwanafunzi anapotumia lugha katika mazingira halisi. Aina hiyo ya majaribio huzingatia majukumu ya mwanafunzi atakayokuwa nayo katika mazingira (jamii) halisi. Majaribio hayo humtayarisha mwanafunzi kumudu majukumu hayo kwa ustadi mkubwa. Kwa mfano, mwanafunzi anayetaka kufanya kazi katika ubalozi wa nchi yake, na jukumu lake kubwa ni ukalimani na tafsiri, basi mbinu za kumfundisha mwanafunzi wa aina hii na vivyo hivyo, majaribio yanayomfaa yatakuwa tofauti na kwa mfano, mwanafunzi anayetaka kujua lugha ya Kiswahili ili awe muhubiri wa masuala ya dini hapa nchini. Aidha, mbinu za ufundishaji na aina ya mazoezi apewayo mwanafunzi anayetaka kuwa mtaalamu wa isimu na lugha ya Kiswahili hana budi kupewa mazoezi yaliyo tofauti na yale tuliyoeleza kwanza. Kwa jumla, ufundishaji lugha ulenge katika kumsaidia mwanafunzi kukuza umilisi wa mawasiliano katika lugha lengwa, na kumudu au kukidhi matarajio yake.

Wataalamu Canale na Swain (1980) waliorodhesha vipengele vinne vya ustadi wa kimawasiliano ambavyo ni:

(a) Ustadi wa kisarufi-ujuzi wa mfumo wa sarufi, yaani fonolojia, mofolojia na sintaksia;
(b) Ustadi wa kiisimu jamii-ujuzi wa kanuni za utumizi wa lugha kwa kuzingatia matumizi sahihi ya lugha katika mazingira fulani;
(c) Ustadi wa kimkakati, yaani uwezo wa kutumia njia mbadala katika mazingira ambapo kuna uwezo pungufu wa utumizi wa lugha ya pili kwa kutumia njia mbadala inayofaa;
(d) Ustadi katika utumizi mpana wa lugha- uwezo wa kutumia lugha katika mazingira mapana kama vile hotuba, mihadhara n.k. Huu ni uwezo wa kutumia lugha kwa kuzingatia mshikamano na mfungamano wa hoja.

Pamoja na kuzingatia vipengele vya ustadi wa kimawasiliano swali la kujiuliza ni je, katika majaribio tupime stadi moja baada ya nyingine au zipimwe zaidi ya moja katika jaribio moja. Kwa hakika hapa kuna misimamo ya aina nyingi. Baadhi ya wanataaluma wanadai kuwa ni vyema kupima stadi moja katika jaribio na si mchanganyiko wa stadi zaidi ya moja. Wengine wanadai kuwa si rahisi kupima stadi moja katika jaribio moja na hivyo, ni vyema kupima stadi zaidi ya moja (Rivers, 1968). Kwa hakika si rahisi kuwa na mtazamo mmoja kuhusu jambo hili kwa kuwa katika kila jaribio malengo ya wanafunzi lazima yafikiriwe. Ni vyema mwalimu akachanganua vipengele kadhaa vya stadi anavyolenga kuvipima kimoja baada ya kingine. Aidha, mwalimu anaweza

kupima vipengele viwili au vitatu vinavyoimarishana na kuendana, kipengele kimoja kikijengwa na kukijenga kipengele kingine. Kwa ujumla, majaribio yetu yanapaswa kulenga katika kumsaidia mwanafunzi na mwalimu kufikia hatua ya kiwango cha juu cha stadi lengwa.

Katika madarasa ya Kiswahili majaribio huwa ama ya kujaza nafasi zilizoachwa wazi, kuchagua jibu sahihi kati ya majibu kadhaa, kuteua jibu lililo kweli au lisilo kweli, kuoanisha majibu, insha n.k. Katika sehemu inayofuata tutatafakari na kutathmini aina za majaribio ambayo tumekuwa tukitayarisha katika madarasa yetu.

Tafakuri na tathmini ya majaribio inayofanyika hapa ina lengo kuu la kupima ustadi wa lugha kimawasiliano. Mojawapo ya majaribio yanayotathminiwa hapa ni uandishi wa insha, kama inavyoonekana katika mfano wa swali lifuatalo:

**SWALI**
Andika insha fupi kuhusu safari yako ya Zanzibar (Write a short essay about your Zanzibar trip)

..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................


*Chanzo: Mtihani wa Kiswahili wa kumaliza Kiwango cha awali Chuo Kikuu cha Georgetown, (Marekani)tarehe 3/8/2009-* (swali la nne)

Hili ni swali mojawapo, katika mtihani uliotajwa, ambalo lengo lake ni kumpa mwanafunzi nafasi ya kuonesha stadi zake za lugha kwa njia ya insha. Hapa mwanafunzi anatarajiwa kuonesha amejifunza msamiati kwa kiwango gani pamoja na utumizi wake wa lugha bila kujifunga na usahihi wa sarufi (ingawa ustadi wa sarufi utajionesha bila kulazimishwa kutumia miundo fulani aitakayo mwalimu). Aina ya maswali yanampa nafasi mwanafunzi kutumia msamiati anaoufahamu na kuonesha uhusiano wa msamiati aliotumia. Hakika swali la aina hii humsaidia mwalimu kugundua ayajuayo mwanafunzi badala ya mwalimu kutaka ajue aina fulani ya muundo au msamiati. Jambo la kuzingatia kwa upande wa mwalimu, hususan katika usahihishaji, ni kutompunguzia alama mwanafunzi aliyeonesha juhudi za kutumia lugha kwa mapana yake badala ya kuandika machache na kupata alama nzuri. Kimantiki kazi finyu itakuwa na makosa machache.

Aina nyingine ya maswali inayokaribiana na hiyo ni kumpa nafasi mwanafunzi ya kujieleza huku ukimpa mipaka ya utumizi wa msamiati mpya ambao atakuwa amejifunza darasani.

**SWALI**

Msichana JoAnn ana mipango mingi ya kufanya wakati wa wikiendi. Tazama picha ya mawazo yake halafu eleza anafikiria kufanya nini.



(Picha inayohusika inaonesha kuna keki, kamera, chupa za mvinyo, vifurushi vya zawadi, barua za mwaliko n.k.

..............................................................................................

..............................................................................................

..............................................................................................

..............................................................................................

*Chanzo: Mtihani wa kupima kiwango cha uelewa wa lugha ya wanafunzi (picha inatokana na mtihani mmojawapo wa Kijapani, swali la pili) toka Chuo Kikuu cha Stanford Marekani (STANFORD African Studies Centre, 2000)*

Mtihani huu hufanywa na wanafunzi kutoka Marekani ambao huja na viwango vya Kiswahili ngazi ya pili au ya tatu. Aina hii ya mitihani hutumika kupima kiwango cha uelewa wa lugha cha mtahiniwa ili aungane na wanafunzi wenzake ambao wanakadiriwa kuwa katika kiwango kimoja wanapoanza masomo ya Kiswahili. Aina hii ya jaribio hupima uwezo wa jumla wa utumizi wa lugha badala ya kupima vipengele mahsusi vya lugha. Kama inavyoonekana katika jaribio hili, hakuna kipengele mahsusi kinachopimwa licha ya kutumia msamiati ulipendekezwa na kuueleza kwa namna ya kiwango cha mhusika. Katika jaribio hili suala la utamaduni limezingatiwa kwa kuwa masuala ya kusherehekea sikukuu za kuzaliwa ni muhimu sana Marekani na hivyo, mwanafunzi anatarajiwa kurejelea utamaduni huo. Hapa mwanafunzi anatumia msamiati huo katika muktadha. Mwanafunzi anapewa fursa ya kuibua mawazo na kuyaoanisha na msamiati wa vifaa mbalimbali vitakavyotumika katika kusherehekea siku hiyo ya kuzaliwa. Lililozingatiwa hapa ni kumpa mwanafunzi mada inayofungamana na yale ayapendayo na ayajuayo na kuibua hisia chanya. Uibuzi wa hisia hizo unamwezesha mwanafunzi kupata mtiririko wa lugha unaojitokeza kwa urahisi kwa kuwa anaandika juu ya mada aijuayo na ni sehemu ya maisha yake. Ni mada inayomfurahisha. Hivyo, si vyema kumtaka mwanafunzi kuelezea mada ambayo haivutii na haina uhalisia kwake.

Sehemu inayofuata inazingatia baadhi ya majaribio ambayo yanaweza kumkwamisha mwanafunzi anayejifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Jaribio mojawapo ni la kujaza nafasi zilizoachwa wazi. Aina hii ya majaribio ina miundo tofauti. Mwanafunzi hupewa majibu yaliyochanganywa na hutakiwa kuteua jibu sahihi. Wakati mwingine anapaswa kujaza jibu ajualo linaloendana na usahihi wa tungo husika na wakati mwingine hutakiwa kurekebisha jibu alilopewa ili liendane na muktadha wa sentensi husika. Jaribio kama hili, kwa mfano, lilifanywa na wanafunzi wa programu ya *Associated Colleges of the Mid West* (ACM) tarehe 8/9/2006 nchini Tanzania kama linavyoonekana hapa chini:

***Jaza nafasi zilizo wazi kwa kutumia viambishi vya mahali***
**(*Fill in the blanks using locative suffixes*)**

| | | |
|---|---|---|
| (a) | *Rafiki yangu.................................* | *Kenya* |
| (b) | *Maembe.......................................* | *Kabatini* |
| (c) | *Basi kubwa...............................* | *hapa* |
| (d) | *Kitabu chako.........................* | *mezani hakimo chumbani* |
| (e) | *Dereva.....................................* | *Ulaya* |

Aina hii ya jaribio inalazimisha mwanafunzi kukumbuka *viambishi vya mahali* na kuvitumia katika "muktadha" sahihi. Hata hivyo, tatizo la jaribio la aina hii ni kuwa mwanafunzi anaweza akabahatisha majibu lakini katika muktadha halisi akashindwa kutumia *viambishi vya mahali* kwa usahihi. Jaribio alilopewa

liko katika mazingira ya kipekee na halizingatii uhalisia wa utumizi katika muktadha halisia. Jaribio linalolenga kukuza stadi ya mawasiliano linahitaji wanaojaribiwa watende kazi halisi ambayo inatumika katika mazingira halisi ya mawasiliano. Jaribio hilo hapo juu halina uhalisia kwa kuwa hakuna mahali ambapo wanafunzi atahitajika kutumia *viambishi vya mahali* katika mazingira ya kipekee. Aidha, inawezekana mwanafunzi akashindwa kung'amua maana halisi ya istilahi ya *viambishi vya mahali* katika lugha lengwa na pia hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya Kiingereza na Kiswahili kuhusu viambishi vya mahali. Pamoja na hayo, hakuna sababu ya msingi ya kujua istilahi za kiisimu za viambishi vya mahali bali lililo muhimu ni utumizi wa viambishi hivyo katika mazingira halisi. Jaribio la kujaza nafasi ambalo linakaribia uhalisia ni kama lioneshwalo hapa chini:

**SEHEMU YA KWANZA**

A. **Chagua maneno kutoka katika kisanduku na kujaza nafasi zilizo wazi ili kuleta mtiririko wa maana katika kifungu kifuatacho.** *(From the box below choose the appropriate words (vocabularies) to make a meaningful flow in the following passage. Write your answers in the space provided)*:

**(10 marks)**

Shagazi (i) ____________ jana, alitaka kununua (ii) ____________ yake. Muuza duka akamwambia kuwa (iii) ________ na mahitaji yote. Yeye alikuwa na sukari, (iv) ____________ nyumbani hakuwa navyo. (v) muda mfupi akasema, tafadhali sina mahitaji yako. Je unataka nini (vi) ________? Shanazi (vii) ____________ kitu kingine chochote. Akajibu, basi (viii) ____________ mahitaji yangu (ix) ____________ nyingine (x) ________ tutaonana siku nyingine.

| | | |
|---|---|---|
| sikuwa<br>baada ya<br>aliyefika<br>kwaheri<br>vya<br>cha | salama<br>hakuwa<br>nitanunua<br>muuza duka<br>hakutaka<br>mwa | vijiji<br>siku<br>zaidi<br>mahitaji<br>uhitaji |

(i) ____________
(ii) ____________
(iii) ____________
(iv) ____________
(v) ____________

(vi) ____________________

(vii) ____________________

(viii) ____________________

(ix) ____________________

(x) ____________________

Chanzo: *Kiwango cha juu-kati Chuo Kikuu cha Princeton*, 13/7/2007

Jaribio hili linaweza pia kumkwaza mwanafunzi lakini lina unafuu tofauti na jaribio lililotangulia. Jaribio hili lina uhalisia wa utumizi wa mazingira yanayoibua maana tumizi. Baada ya kujaza nafasi zilizo wazi panatokea mtiririko wa aya ambao ni halisia na inawezekana maudhui yaliyomo katika aya hiyo yameshuhudiwa na wanafunzi katika mazingira halisi. Wanafunzi watakuwa wamekwisha nunua vitu kadhaa dukani. Aidha, lililolengwa katika jaribio hili ni utumizi wa msamiati na sarufi na lengo hilo limefikiwa.

Aina nyingine ya jaribio ambalo halifai kutumika kwa wanafunzi kama halikutungwa vizuri ni jaribio la kuoanisha majibu kama linalooneshwa hapa chini (Kiwango cha kati ACM, 8/9/2006):

Husianisha maneno ya kundi A na yale ya kundi B
Match the words in group A to the words in group B

| | | | |
|---|---|---|---|
| (a) | gari, boti, basi, treni | (i) | maziwa |
| (b) | radio, televisheni, magazeti | (ii) | rangi |
| (c) | kalamu, daftari, kalamu, kitabu | (iii) | mikoa ya Tanzania |
| (d) | mchungwa, mwembe, mpapai | (iv) | vyombo vya habari |
| (e) | Zanzibar, Changuu, Pema | (v) | vyombo vya bahari |
| (f) | Kilimanjaro, Meru, Evarest, Himalaya | (vi) | vifaa vya mwanafunzi |
| (g) | Ontario, Tanganyika, Victoria | (vii) | hisia |
| (h) | bluu, kijani, nyekundu, kahawia | (viii) | miti ya matunda |
| (i) | Dar es Salaam, Dodoma, Arusha | (ix) | milima |
| (j) | chukia, furahi, sikitika, choka | (x) | visiwa |

Wanafunzi hujibu jaribio la aina hii kwa kuteua majibu sahihi yanayooana na fasili iliyotolewa. Maswali ya aina hii yanatumika kupima utambuzi na kumbukumbu. Tofauti na yale yaliyotangulia, maswali ya aina hii hayampi fursa mwanafunzi ya kufanya mazoezi katika muktadha halisi. Kinachotokea ni kumlazimisha mwanafunzi "kukariri" uhusiano wa msamiati, yaani msamiati mmoja kuhusishwa na maneno kadhaa. Laiti kama zoezi hili lingeandikiwa aya fulani inayoibua uhusiano huo wa maneno, basi jaribio la namna hiyo angalau lingekuwa linazingatia utumizi halisi. Pamoja na upungufu huo, wazo la jaribio

la aina hii linamwezesha mwanafunzi kuelewa uhusiano na hata matumizi ya msamiati fungamanishi.

Majaribio mengine yanayoweza kutumika ni yale ya uteuzi wa jibu sahihi kutoka katika majibu mengi. Aina hii ya majaribio husifiwa na baadhi ya wataalamu kama asemavyo McNamara (2000) kuwa ni majaribio muhimu kati ya majaribio ambayo yanakuwa na muundo wa majibu. Hata hivyo, yeye anapendekeza aina hiyo ya jaribio kupima usikilizaji. Utumizi wa lugha kimawasiliano unalenga kupima ujuzi wa mwanafunzi kuhusu lugha na uwezo wake wa kuitumia lugha katika mazingira halisi ya lugha lengwa (Bruck, 2001 na Weir, 1990).

Aina ya mwisho ya, jaribio tunalotaka kutolea mfano ni lile linalohusu tafsiri. Tazama swali lifuatalo, kwa mfano:

A: ***Tafsiri sentensi zifuatazo katika Kiswahili***
(***Change the following sentences into Swahili***) (***2 marks each***)

1. *This is my small table clock which I bought in Karikoo*

   ________________________________________

2. *I am teaching you (to be in one verb) to cook good rice.*

   ________________________________________

3. *Before eating you must wash your hands.*

   ________________________________________

4. *Do not take photograhs here.*

   ________________________________________

5. *You made me drinking water but not cold tea.*

   ________________________________________

**Chanzo**: *Mtihani wa wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Georgetown, sehemu ya Mtihani*; *Kiwango cha juu, Juni 21, 2011*

Pametolewa mawazo mbalimbali kuhusu ubora na udhaifu wa tafsiri kama nyenzo ya kufundishia lugha. Hata hivyo, mawazo mengi yanaelezea udhaifu mkubwa wa majaribio ya tafsiri. Lado (1964) anatoa vipengele saba dhidi ya majaribio ya tafsiri kama njia ya kupima uhodari wa stadi kuu nne za lugha. Anaeleza kuwa tafsiri:

(i) Haitumiwi na wanafunzi hodari;
(ii) Ina njia mbalimbali za kutafsiri na kutathmini tafsiri;
(iii) Usahihishaji wake ni mgumu na hauaminiki;
(iv) Huchukua muda mrefu kufanywa na wanafunzi;
(v) Ni stadi maalumu tofauti na kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kuandika;
(vi) Huchukua muda mrefu kusahihishwa;

(vii) Majaribio ya tafsiri huchochea matumizi mabaya ya tafsiri darasani.

Pamoja na kasoro za majaribio yanayowalazimisha wanafunzi kutafsiri, inawezekana kukawa na kundi la wanafunzi ambao lengo lao ndio hilo. Hivyo zoezi la namna hiyo ni muhimu kwao.

Kwa wanafunzi wa kiwango cha kati na cha juu, majaribio bora hayana budi kuibua dhima kuu mbalimbali za lugha ambazo ni pamoja na kutoa na kupokea taarifa. Majaribio hayo yalenge katika kutoa taarifa ya hali ya mambo yalivyo, hali ya ujuzi uliopo na/au uliopita, hali ya mipango ya baadae, na kadhalika. Majaribio yaweza pia kuibua uwezo wa kueleza maoni, kuyatetea maoni hayo au pia kuyalinganisha na kuyalinganua. Majaribio yalenge pia katika kumpa mazoezi wanafunzi ya kumwezesha kufupisha yale anayotaka kusema na kuweza kuelezea yale anayoyapendelea zaidi kuliko mengine.

Pamoja na mapendekezo hayo, tunatambua ugumu wa kutenganisha stadi mbalimbali za lugha. Kwa mfano, ni vigumu kutenganisha stadi ya kuzungumza na ile ya kusikiliza. Stadi hizo zinafungamana. Hivyo basi, majaribio wakati mwingine yasaidie katika kumzoeza mwanafunzi kuoanisha stadi mbalimbali zilizomo katika jaribio moja. Aidha, tunatambua pia kuwa si rahisi kuwa na mazoezi ya utendaji kwani wakati mwingine katika mawasiliano vipengele vingine havipimiki, kwa kuwa vinazingatia uandishi tu. Kumfanya mwanafunzi asitumie mawazo fulani au ayabadilishe kutokana na muono wa uso wa mzungumziwa, hali ya namna hiyo haiwezi kufanyika katika jaribio la uandishi hata kama yanayozungumzwa ni halisi.

**4.0 Mjadala**

Tulichoibua katika makala haya ni kusisitiza kigezo kikuu cha majaribio bora, ambacho ni kupima utendaji wa matumizi ya lugha katika mazingira halisi. Aina hii ya upimaji imetajwa na Spolsk (1984) kuwa inaangukia katika kipindi cha upimaji wa utumizi wa lugha, alichokiita "isimusaikolojia- isimujamii. Katika kipindi hiki hiki malengo ya majaribio yalikuwa, si tu kupima maarifa ya lugha inavyofanya kazi bali hasa kupima uwezo wa watumiaji lugha. Kwa hakika Spolsky (1989:40) alidai kuwa "majaribio ya lugha yahusishe upimaji wa maarifa ya lugha na matumizi ya lugha (Tafsiri na mkazo ni wetu).

Kwa jumla, wazo kuu lililoibuliwa katika makala haya ni lengo kuu la kujifunza lugha ambalo ni mawasiliano. Vivyo hivyo, juhudi kubwa ilikuwa ni kulenga katika mjadala wa jinsi ya kufumbata utendaji wa kupima umilisi wa mawasiliano. Umilisi huo unapendekezwa, kwa mfano na Swain (1980:29) kuwa wa ana tatu. Aina ya kwanza ni umilisi wa kisarufi ambao unahusisha "maarifa ya msamiati na kanuni za mofolojia, sintaksia, sarufi ya sentensi na

(vii) Majaribio ya tafsiri huchochea matumizi mabaya ya tafsiri darasani.

Pamoja na kasoro za majaribio yanayowalazimisha wanafunzi kutafsiri, inawezekana kukawa na kundi la wanafunzi ambao lengo lao ndio hilo. Hivyo zoezi la namna hiyo ni muhimu kwao.

Kwa wanafunzi wa kiwango cha kati na cha juu, majaribio bora hayana budi kuibua dhima kuu mbalimbali za lugha ambazo ni pamoja na kutoa na kupokea taarifa. Majaribio hayo yalenge katika kutoa taarifa ya hali ya mambo yalivyo, hali ya ujuzi uliopo na/au uliopita, hali ya mipango ya baadae, na kadhalika. Majaribio yaweza pia kuibua uwezo wa kueleza maoni, kuyatetea maoni hayo au pia kuyalinganisha na kuyalinganua. Majaribio yalenge pia katika kumpa mazoezi wanafunzi ya kumwezesha kufupisha yale anayotaka kusema na kuweza kuelezea yale anayoyapendelea zaidi kuliko mengine.

Pamoja na mapendekezo hayo, tunatambua ugumu wa kutenganisha stadi mbalimbali za lugha. Kwa mfano, ni vigumu kutenganisha stadi ya kuzungumza na ile ya kusikiliza. Stadi hizo zinafungamana. Hivyo basi, majaribio wakati mwingine yasaidie katika kumzoeza mwanafunzi kuoanisha stadi mbalimbali zilizomo katika jaribio moja. Aidha, tunatambua pia kuwa si rahisi kuwa na mazoezi ya utendaji kwani wakati mwingine katika mawasiliano vipengele vingine havipimiki, kwa kuwa vinazingatia uandishi tu. Kumfanya mwanafunzi asitumie mawazo fulani au ayabadilishe kutokana na muono wa uso wa mzungumziwa, hali ya namna hiyo haiwezi kufanyika katika jaribio la uandishi hata kama yanayozungumzwa ni halisi.

**4.0 Mjadala**

Tulichoibua katika makala haya ni kusisitiza kigezo kikuu cha majaribio bora, ambacho ni kupima utendaji wa matumizi ya lugha katika mazingira halisi. Aina hii ya upimaji imetajwa na Spolsk (1984) kuwa inaangukia katika kipindi cha upimaji wa utumizi wa lugha, alichokiita "isimusaikolojia- isimujamii. Katika kipindi hiki hiki malengo ya majaribio yalikuwa, si tu kupima maarifa ya lugha inavyofanya kazi bali hasa kupima uwezo wa watumiaji lugha. Kwa hakika Spolsky (1989:40) alidai kuwa "majaribio ya lugha yahusishe upimaji wa maarifa ya lugha na matumizi ya lugha (Tafsiri na mkazo ni wetu).

Kwa jumla, wazo kuu lililoibuliwa katika makala haya ni lengo kuu la kujifunza lugha ambalo ni mawasiliano. Vivyo hivyo, juhudi kubwa ilikuwa ni kulenga katika mjadala wa jinsi ya kufumbata utendaji wa kupima umilisi wa mawasiliano. Umilisi huo unapendekezwa, kwa mfano na Swain (1980:29) kuwa wa ana tatu. Aina ya kwanza ni umilisi wa kisarufi ambao unahusisha "maarifa ya msamiati na kanuni za mofolojia, sintaksia, sarufi ya sentensi na

fonolojia." Aina ya pili ni umilisi wa kiisimu-jami ambao unahusisha kanuni za matumizi ya lugha kwa kuzingatia utamaduni wa jamii na kanuni za kilongo. Aina ya tatu ya umilisi ni ya kimkakati inayohusu mbinu za mazungumzo na matendo ambayo hutumiwa na mzungumzaji anapokuwa anaziba viraka katika mazungumzo yanayoweza kutokea kutokana na kupwaya kwa umilisi wa lugha. Baadhi ya vipengele vingine vinavyohusishwa na umilisi wa lugha kiutendaji ni pamoja na uhodari wa usukaji hoja na uzingatizi wa pragmatiki.

Kwa wanafunzi wageni wanaojifunza Kiswahili, kama lugha yao ya pili na wanaotoka nje ya nchi, kwa mfano, majaribio yao yanaweza kulenga katika utumizi wa lugha kuzungumza na dereva wa teksi kutoka uwanja wa ndege, mazungumzo na muuza fedha za kigeni katika maduka ya fedha za kigeni, mazungumzo na waangalizi wa kastamu, mazungumzo ya hotelini, na kadhalika. Matumizi ya lugha katika shughuli za aina hii, majaribio yalenge katika kupata uthabiti na utumizi wa lugha katika stadi za uhalisia wa maisha.

Changamoto nyingine ni pamoja na muda. Jaribio hupewa muda maalumu kumalizika. Muda huo inawezekana kabisa hauendani na mwanafunzi ambae anafanya kazi polepole lakini kwake kila hatua ni muhimu na humsaidia kuibua uhalisia wa kiwango chake cha matumizi ya lugha. Aidha, suala la mawasiliano na makabiliano katika matumizi halisi, kila tamko lina kusudio, kwa hiyo, ni vigumu kuelezea kusudio katika ombwe. Hivyo, kihalisia majaribio yanakuwa nje ya muktadha halisi hata kama muktadha ni wa kufikiria. Halikadhalika, utumizi wa stadi na mfungamano wa stadi hizo kwa wakati mmoja ni vigumu kuupima. Mwanafunzi anaweza kumudu stadi zote kipwekepweke lakini akashindwa kuzitumia katika mazingira halisi. Kwa kuzingata hayo, kuna umuhimu wa kutunga majaribio ambayo yanamweka mwanafunzi katika mazingira halisi. Kwa mfano, majaribio ya kuigiza daktari na mgonjwa yanaweza kuwa ya manufaa kuliko kujieleza katika maandishi tu.

Pamoja na malengo hayo ya majaribio, kuna changamoto ambazo watahini wataweza kukabiliana nazo. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na kutokuwa na kipimo kamili kati ya ubora na wingi wa majaribio. Hapa hisia za wapimaji zinaweza kutumbukia kiasi cha kuleta tofauti kati ya mpimaji mmoja na mwingine au kundi moja la wapimaji na lingine. Hili pia linaendana na ugumu wa kupima usahihi wa maudhui ya majaribio. Ni kwa kiwango kipi cha juu au cha chini cha ubora wa kazi moja na nyingine hata katika muktadha halisi. Hili ni wazo ambalo linahitaji utafiti zaidi.

Licha ya hoja hizo za jumla, changamoto iliyo mbele yetu ni kuwa na majaribio ya kimataifa katika Kiswahili. Wakati umefika wa kuchukua hatua pamoja na kushirikisha vyuo vya nje vinavyofundisha Kiswahili kwa kuandaa majaribio

(mitihani) yanayopima viwango vya kimataifa. Katika kufanya hivyo, tutakuwa tumekiinua Kiswahili katika viwango vya Kimataifa. Pamoja na kubukua wafanyavyo wenzetu wa lugha kongwe za kimataifa wanapotahini uwezo wa wanafunzi wageni wa lugha hizo, pana haja basi ya kufanya utafiti wa kina ili kubaini masuala yapi katika majaribio hayo yatiliwe mkazo na kwa kiwango gani.

**5.0 Hitimisho**

Katika makala haya tumetafakari masuala ya msingi ya kuzingatia katika utungaji wa majaribio bora yanayozingatia vipimo bora na ambavyo, kwa ujumla wake, vinamuendeleza mjifunzaji wa lugha. Masuala ya utendaji katika utayarishaji wa majaribio yameelezwa. Kilichojitokeza bayana ni kuwa utungaji wa majaribio, ni suala linalohitaji umakini wa hali ya juu unaozingatia uaminikaji, uthibitikaji, uhalisia, uhusianifu, matokeo na utekelezaji. Umuhimu wa kulenga vipimo hivyo ni kuwa na mchakato wa utayarishaji wa majaribio wenye maamuzi yakinifu yanayohusisha upangaji, utayarishaji na uchambuzi wa majaribio hayo. Majaribio yasitungwe kama jambo la dharura, bali yahusishwe na malengo ya walengwa na matarajio yao. Katika kufanya hivyo majaribio yanaweza kuwa nyenzo ya ujifunzaji na ufundishaji wa lugha na yatakidhi maadili ya upimaji. Mwisho tumependekeza kwamba kuna haja ya kuanzisha majaribio ya Kiswahili ili kupima viwango vya uelewa katika ngazi ya Kimataifa.

## Marejeo

Bachman, L.F. na A.S. Palmer, (1996). *Language testing in Practice*. Buck: Oxford University Press.

Brown, H.D. (2004). *Language assessment: Principles and classroom practices.* Person Education, Inc.

Canale, M. na M. Swain, (1980). "Theoretical base of communicative aproach to second language teaching and testin."Katika *Applied Linguistics* Juz. 1, uk. 1-47.

Carford, J.C. (1965). *A Linguistic Theory of Translation*. Oxford: Oxford University Press.

Cunningham, G.K. (1998). *Assessment in the Classroom.* Bristol, P.A: Falmer Press.

Fulcher G. (2010). *Practical language Teaching:* London: Hodder Education.

Lado, R. (1964). *Language Teaching: A scientific approach.* New York: McGraw-Hill.

McNamara, T. (2000). *Language testing.* Oxford: Oxford University Press.

Rubanza, Y.I. (1997). "Teaching Kiswahili as a Foreig Language in Target Country: A Thouought on Culture Aspect." A paper presented at the African Language Teachers Association. Madison Wisoconsin, U.S.A.

Spolsky W.A.W. na M. Murray-Ward, (1999). *Assessment in the Classroom*, Belmont CA: Wadsworth Publishing Co.

Weir, C.J. (1990/2004). *Language Testing and Validation: An Evidence Based Approach*. Basingstoke: Palgrave.

Widdowson, H.G. (1978). *Teaching Language as Communication*. Oxford: Oxford University Press.